**HOTUBA YA KATIBU KIONGOZI, BALOZI OMBENI Y. SEFUE, KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA SERIKALI MTANDAO KATIKA UKUMBI WA ARUSHA INTERNATIONAL CONFERENCE CENTRE (AICC) – ARUSHA, TAREHE 19 AUGUST, 2015**

---

***Ndugu Makatibu Wakuu;***
***Naibu Makatibu Wakuu;***
***Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Serikali Mtandao;***
***Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali;***
***Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi Mbalimbali za Taasisi za Serikali;***
***Watoa Mada;***
***Wageni Waalikwa;***
***Wana Habari;***
***Mabibi na Mabwana.***

***Habari za Asubuhi!***

Ninapenda kuwashukuru wote waliohusika katika kuandaa mkutano huu muhimu na wa kwanza wa aina yake. Kipekee nakushukuru Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ndugu HAB Mkwizu, pamoja na wenzako kwa maandalizi haya na kwa kunialika kujumuika nanyi kwenye ufunguzi wa mkutano huu.

Nawashukuru pia watoa mada wote, wakiwemo wageni wetu kutoka India na Singapore, kwa kukubali kujumuika nasi na kuchangia ujuzi, maarifa na uzoefu wao mkubwa katika masuala mbalimbali yanayohusu Serikali Mtandao. Nchi zenu zimepiga hatua kubwa sana katika eneo hili na nyie ni sehemu ya mafanikio hayo. Hivyo, tuna fursa kubwa ya kujifunza mengi kutoka kwenu kwenye eneo hili. Karibuni sana.

***Ndugu Washiriki na Wageni wetu,***

Nimejulishwa kuwa mkutano huu umehudhuriwa na Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Watendaji Wakuu, Wakurugenzi Wakuu, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Wajumbe wa Bodi ambao ndio watoa maamuzi kwenye taasisi husika. Nafahamu pia kuwa mkutano huu umefuatia mkutano wa aina hii uliofanyika kwa siku mbili zilizopita na kuwahusisha Wakurugenzi na Wakuu wa Idara za Mipango, TEHAMA pamoja na Usimamizi na Menejimenti ya Rasilimaliwatu; watalaam wa TEHAMA Serikalini na Maafisa Habari, ambao ni watekelezaji wa maamuzi mbalimbali kwenye taasisi zao.

Matarajio yangu ni kuwa mkutano huu utakuwa chachu ya kutoa msukumo mpya wa utekelezaji wa malengo ya Serikali Mtandao, ikiwemo kwa kujenga uwezo ndani ya Serikali na taasisi zake.

Mkutano huu ni moja ya mikakati ya kujenga na kuboresha uwezo huo kwa kuimarisha mawasiliano miongoni mwa wadau, kubadilishana uzoefu na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA yenye tija katika kuboresha utendaji wa taasisi za umma na kutatua changamoto za utendaji wa taasisi hizo.

***Ndugu, Washiriki***

Dhana ya Serikali Mtandao na utekelezaji wake ni sehemu ya maboresho ya Utumishi wa Umma ambayo yana historia ndefu katika nchi yetu. Kwa nyakati tofauti, Tanzania imekuwa ikifanya maboresho ya kisiasa, kiuchumi na kiutawala kwa lengo la kuboresha utendaji na kuongeza uwajibikaji ili kufikia malengo ya maendeleo ya nchi.

Maboresho haya yalipata msukumo mpya katika miaka ya 1990 na tangu wakati huo Serikali imekuwa ikitekeleza kwa awamu maboresho ya kisera, kisheria, kiutaratibu na kimfumo katika sekta ya Utumishi wa Umma. Lengo lilikuwa kuhakikisha kwamba Serikali inatimiza lengo lake la kuwahudumia wananchi kwa ukamilifu na, zaidi, kwa wakati.

Kati ya mwaka 1993 na 1999 Serikali ilitekeleza maboresho ambayo yaliitwa Mpango wa Kuboresha Utumishi Serikalini (*Civil Service Reform Programme*). Awamu hii ya Maboresho ililenga, pamoja na mambo mengine, katika kupunguza matumizi ya Serikali kwa kurekebisha muundo wa Serikali na kupunguza idadi ya watumishi wake.

Kuanzia Mwaka 2000 na kuendelea, Serikali iliendelea na awamu nyingine ya maboresho kupitia Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma (*Public Service Reform Programme* - PSRP) ambayo, pamoja na mambo mengine, ilikusudia kuweka Mifumo ya Kusimamia Utendaji (*Perfomance Management Systems*), kuboresha huduma zinazotolewa kwa umma na kujenga uwezo wa watumishi wake wa kutoa huduma hizo.

Maboresho haya yalilenga kuleta mabadiliko makubwa (*paradigm shift*) katika utendaji wa shughuli za Serikali, kuongeza uwajibikaji na kuwa na Utumishi wa Umma wenye mfumo unaofanana (*Unified Public Service*). Matumizi ya TEHAMA katika kuboresha utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa umma yalikuwa ni sehemu ya maboresho haya. Hata hivyo, mabadiliko haya hayakuhusisha mikakati madhubuti na ya muda mrefu ya kuifanya TEHAMA kuwa chombo cha kuboresha utendaji Serikalini.

***Ndugu Washiriki,***

Nimetoa utangulizi huu ili kuondoa wasiwasi miongoni mwenu na wadau wengine kwamba Serikali Mtandao ni dhana mpya ambayo pengine inahitaji rasilimali nyingi, uwekezaji mkubwa na utalaamu wa hali ya juu miongoni mwa taasisi za umma.

Kwa ufupi, Serikali Mtandao ni matumizi ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika utendaji kazi Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za utendaji na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Serikali Mtandao siyo teknolojia pekee kama wengine wanavyoichukulia bali ni matumizi ya TEHAMA ili kuboresha utendaji kazi wetu wa kila siku (*Government Business Process Improvement*).

***Ndugu Washiriki,***

Tangu tuamue kubuni mipango na mikakati madhubuti ya kutumia TEHAMA kuboresha utendaji, naamini sote tumeona manufaa yake. Kwa hakika

tumepiga hatua ya kuridhisha katika utekelezaji wa Serikali Mtandao. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana, mbali na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya TEHAMA, ni pamoja na;

- Kuanzishwa kwa Wakala ya Serikali Mtandao (*eGA*) ili kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma;

- Uboreshaji wa sera na sheria, kutokana na kutungwa kwa Sera ya TEHAMA 2003, na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Serikali Mtandao, 2013 (*National e-Government Strategy*); pamoja na Sheria ya "*Electronic and Postal Communications*" 2010, Sheria za Miamala ya Kielektroniki, 2015 (*Electronic Transactions Act, 2015*) na Sheria ya Makosa ya Mitandao, 2015 (*Cybercrimes Act, 2015*);

- Tumefanya uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya TEHAMA, kama vile Mkongo wa Taifa (*NICTBB*), Mtandao wa Serikali (*GovNet*), Vituo vya Kitaifa vya Data (*National Data Centres*), na kutenga Masafa ya Intaneti ya Serikali (*Internet Bandwidth*);

- Tumeweka mifumo tumizi ya kimkakati na kisekta, na kuongeza njia mbadala za kutolea huduma kwa wananchi kwa kutumia TEHAMA, zikiwemo Tovuti Kuu ya Serikali, simu za mikononi na vifaa vingine vya kielektroniki.

Kwa ujumla wake, utekelezaji wa juhudi za Serikali Mtandao umechangia kwa kiasi kikubwa katika kurahisisha utoaji wa taarifa na huduma kwa

wananchi kwa haraka, uwazi, urahisi, gharama nafuu, wakati wowote na mahali popote nchini, na kwa kweli duniani.

***Ndugu Washiriki,***

Napenda kutumia fursa hii kuzipongeza sana taasisi za umma ambazo zimefanikiwa kuboresha utendaji kazi na utoaji huduma zao kwa umma kwa kutumia TEHAMA. Kwa upande wa taasisi za Serikali ambazo bado zina kiwango kidogo cha utekelezaji wa Serikali Mtandao, kuna mambo mawili, badilikeni au mtabadilishwa. Chukueni hatua za haraka ili kuhakikisha mnatumia fursa zitokanazo na matumizi ya TEHAMA katika kuboresha ufanisi na utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Na kila wakati, shirikianeni na Wakala ya Serikali Mtandao ili tuwe na Serikali Mtandao madhubuti. Ahadi yangu ni kuwa Serikali itaendelea kutoa msukumo mkubwa kwenye jambo hili.

***Ndugu Washiriki,***

Licha ya mafanikio tuliyoyapata, ni vema tuendelee kukumbushana wakati wote kwamba eneo hili bado linakabiliwa na changamoto kadhaa za kisera, kimuundo na kiutekelezaji. Tutahitaji, kwa mfano kuwa na sera na sheria mahsusi inayosimamia Serikali Mtandao ili kuzifanya taasisi za Serikali kuwa na muono na malengo yanayoshabihiana katika matumizi ya TEHAMA. Vile vile tunahitaji kuwekeza zaidi katika kupata watumishi wenye ujuzi wa kiwango kinachotakiwa ili kukidhi mahitaji ya utekelezaji wa juhudi mbalimbali za TEHAMA zinazoendelea.

***Ndugu Washiriki,***

Miongoni mwa matatizo makubwa tuliyo nayo yanatokana na kukosekana kwa Mfumo mmoja ulio chini ya Chombo au Mamlaka moja katika kutambua na kusajili watu. Hii inakwamisha utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini kutokana na taarifa za mtu mmoja kutofautiana na za mwingine, kuwepo tofauti kati ya mfumo mmoja na mwingine na kutokuwepo kwa uwiano wa kutosha kati ya taratibu za utendaji kazi Serikalini (*business processes*) na teknolojia inayotumika. Matokeo yake:

- Serikali haipati thamani halisi ya fedha zinazotolewa kwenye miradi ya TEHAMA;

- Taasisi za Serikali zinakuwa na mifumo ambayo haiongei na haiwezi kuwasiliana na kubadilishana taarifa (*ndani ya taasisi, na kati ya taasisi na taasisi*);

- Urudufu wa mifumo miongoni mwa taasisi za Serikali yenye viwango tofauti;

- Msukumo na utegemezi wa wakandarasi kwa kiasi kikubwa katika kushauri, kubuni, kusimamia na kuhifadhi mifumo ya TEHAMA ya Serikali;

- Uhusiano na uratibu hafifu wa shughuli za TEHAMA ndani na kati ya Taasisi za Serikali;

- Ukosefu wa njia za kutosha za kutoa huduma za Serikali Mtandao (*service delivery channels*);

- Idadi ndogo ya huduma na taarifa za Serikali zinazotolewa kupitia TEHAMA;

- Kuongezeka kwa matishio ya usalama wa taarifa katika mifumo ya TEHAMA.

***Ndugu Washiriki***

Ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeweka msukumo mpya katika kutekeleza Serikali Mtandao kwa kusisitiza ushirikiano na matumizi ya pamoja ya rasilimali TEHAMA miongoni mwa taasisi za umma, kujenga uwezo wa taasisi za umma na watumishi wake katika matumizi ya TEHAMA, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA, kuimarisha uratibu wa shughuli za TEHAMA na usalama wa taarifa za Serikali. Haya na mengine ambayo sikuyataja, yana lengo la kuongeza tija na ufanisi katika kuiendesha Sekta ya Umma, kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali na kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa muhimu katika kila ngazi na sekta ya Umma.

Kwa nafasi zenu kama viongozi na watendaji wakuu wa taasisi, ni vema na ni lazima kuweka na kutekeleza mikakati kabambe ya namna ya kuzishughulikia changamoto hizi. Nafahamu kwamba changamoto nyingine zinahitaji jitihada za muda mrefu na mtambuka, umiliki wa pamoja wa jitihada hizo, na uelewa wa pamoja kuhusu malengo ya Serikali Mtandao. Hata hivyo, kuna mambo ambayo yapo ndani ya uwezo wa kila taasisi, hivyo, yaanze kufanyiwa kazi hasa yale yanayotoa matokeo ya haraka.

Mfano wa mambo yanayoweza kufanywa ni pamoja na kuhakikisha miradi na mifumo yote inayoanzishwa inakuwa sehemu ya uboreshaji kazi wa taasisi na kwamba inakuwa sehemu ya mipango ya taasisi husika na sio vinginevyo. Kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita, tumeshuhudia mifumo mingi ikiwekwa Serikalini. Kwa kiasi kikubwa mifumo hiyo imekuwa inawategemea wakandarasi katika kuiendesha ambapo Serikali imekuwa ikiingia gharama kubwa na wakati mwingine kuhatarisha usalama wa taarifa zetu. Hivyo, ni vema mkahakikisha mifumo inayowekwa kwenye taasisi zenu haiwafungi au kuwabana na Wakandarasi kama ilivyo sasa kwa baadhi ya mifumo yetu mikubwa bali inakuwa ni mifumo ambayo Serikali yenyewe inaweza kuihudumia na kwa gharama nafuu.

***Ndugu Washiriki,***

Pengine ni muhimu, kwa namna ya pekee kutumia fursa hii kutoa msisitizo mahsusi kuhusiana na changamoto zinazohusiana na suala la usalama mitandaoni. Na kwa minajili hiyo nazitaka taasisi zote za umma kuzingatia viwango vyote vya usalama kwenye mifumo husika zinapotekeleza miradi ya TEHAMA. Ni vema wakati wa kubuni mfumo uoneshe ni namna gani taarifa zitakavyokuwa zinalindwa tangu mwanzo wa mradi badala ya kujenga mfumo kwanza na unapokamilika ndipo unafikiria utalindwaje.

Aidha, utengenezaji wa mifumo yetu uzingatie programu ambazo watalaam wetu wanaweza wakatambua kinachofanyika (*access to source codes*) badala ya kuwa na mifumo ambayo hatujui kinachoendelea nyuma ya pazia.

Kwa mfano, matumizi ya programu huria (*Open Source*) pamoja na kusaidia katika kuhakikisha usalama wa mifumo pia una faida nyingine kama vile kuepuka gharama kubwa ya leseni za uendeshaji pamoja na urahisi wa kuendeleza mfumo husika kwa mahitaji ya taasisi. Ni vema taasisi husika zikawa na uwezo wa ndani kabla ya kutumia programu huria hizi au wahakikishe wanaihusisha Wakala ya Serikali Mtandao kikamilifu ili kuweza kupata utalaam wa kutosha. Ni matumaini yangu kwamba sisi kama wadau, kupitia mkutano huu, tutashirikiana pamoja kutafuta njia za kukabiliana na changamoto hizi.

***Ndugu Washiriki,***

Moja ya majukumu ya Wakala ya Serikali Mtandao ni kuratibu matumizi ya TEHAMA kwenye taasisi za umma. Nimesema sana huko nyuma na nimetoa maelekezo na miongozo. Na leo ninarudia. Ninaziagiza Taasisi zote za Umma kuishirikisha Wakala kila wanapobuni na kutekeleza miradi mbalimbali ya TEHAMA. Hii itasaidia kuondoa urudufu wa miradi mbalimbali ya TEHAMA miongoni mwa taasisi za Serikali. Hatuwezi kuendelea tulivyofanya huko nyuma kabla ya kuanzisha Wakala.

Wakala hii imeanzisha mfumo wa kukusanya taarifa zote za hali ya TEHAMA kwa wakati wote kwenye taasisi za Serikali. Mfumo huu utasaidia kupata taarifa yoyote ya kinachoendelea Serikalini kuhusu TEHAMA. Hivyo, naziagiza taasisi zote za umma kutoa taarifa zote zinazohusu TEHAMA kwenye taasisi kama watakavyoelekezwa ili kuhakikisha kuwa Serikali inakuwa na taarifa zote za TEHAMA zitakazosaidia katika kupanga na kutekeleza miradi mbalimbali ya TEHAMA.

Ni ukweli usiopingika kwamba hakuna sekta yoyote iliyoendelea bila kuratibiwa, kwa hiyo ni vema mkazingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na Wakala katika kutekeleza Serikali Mtandao. Natoa tahadhari kuwa kuanzia sasa Serikali itajumuisha miongozo hiyo kama sehemu ya ukaguzi unaofanywa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mdhibiti wa Hesabu za Serikali. Hivyo, msipozingatia mjue kwamba mtapata hoja za ukaguzi.

Kwa upande wa Wakala ya Serikali Mtandao, naitaka ihakikishe inajenga uwezo wa kutosha na kuweka utaratibu mzuri wa kuzisaidia taasisi za Umma katika matumizi ya TEHAMA na kamwe wasigeuke kikwazo. Fanyeni tafiti za Serikali Mtandao ambazo zitazisaidia taasisi za Umma kuboresha utoaji wa huduma. Aidha, wakati umefika sasa kwa Wakala hii kuweka utaratibu wa kujenga na kuendeleza mifumo shirikishi ambayo itasaidia kuendeleza mifumo iliyopo pamoja na kuibua mifumo mipya. Najua, na nina uhakika, kuwa mnao uwezo wa kufanya hivyo.

***Ndugu Washiriki,***

Kwa kutambua kuwa matumizi sahihi ya TEHAMA ni nyenzo na kichocheo muhimu katika kufikia kwa haraka malengo yetu ya Kitaifa ya Maendeleo tuliyojiwekea ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Programu ya Maboresho ya Sekta ya Umma na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN), nawahakikishia kwamba Ofisi yangu na Serikali kwa ujumla tutaendelea kutoa kipaumbele cha pekee katika utekelezaji wa Serikali Mtandao kwani ni dhana ambayo haikwepeki katika uendeshaji Serikali leo na hasa siku zijazo.

Aidha, Serikali Mtandao itatusidia kuongeza uwazi, uwajibikaji, kupiga vita rushwa na kubana matumizi ya Serikali. Narudia kusisitiza, Ofisi ya Rais,

Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala ya Serikali Mtandao shirikianeni na Tume ya Mipango katika kuhakikisha masuala ya Serikali Mtandao yanaingizwa na kuoanishwa na Mpango wa Serikali wa Miaka Mitano na mipango mingine, si kama jambo la peke yake bali kama nyenzo muhimu ya kufikia malengo yote tutakayokuwa tumejiwekea.

***Ndugu Washiriki,***

Namalizia kwa kuwakumbusha kwamba utekelezaji wa Serikali Mtandao unahitaji muda mrefu na utashi wa pamoja wa viongozi, watendaji, wananchi na wadau wengine. Lakini si jambo la hiari tena; ni jambo la lazima. Serikali imeweka mazingira mazuri ya kisera na kimkakati ili kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA yanakuwa na tija katika kuwahudumia wananchi na kuwaondolea kero mbalimbali. Hatimaye lengo letu ni kufikia malengo ya kitaifa ya kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania.

Hivyo, ningependa msikilize kwa umakini wadau mbalimbali watakaowasilisha mada, mjadili mada hizo kwa uwazi, ukweli na umakini mkubwa ili hatimaye mtoke na mapendekezo yatakayowezesha Serikali kuufanya utoaji wa huduma kwa Umma kupitia TEHAMA uwe bora zaidi, wenye ufanisi, na unaokidhi matarajio ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Mwisho, natarajia kuwa huu hautakuwa mkutano wa kwanza na wa mwisho. Lazima mtafute njia ya kuhakikisha majadiliano haya na kuelimishana huku kunakuwa endelevu. Na, ni muhimu kila mmoja wenu aendelee kushiriki pale mtakapotaarifiwa.

Baada ya kusema hayo sasa natamka kwamba Mkutano wa Mwaka 2015 wa Serikali Mtandao umefunguliwa rasmi.

***Asanteni kwa kunisikiliza.***